# MAYAHUDI HAWAMSADIKI MTUME

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

(MAYAHUDI HAWAMSADIKI MTUME (S.A.W.W

.(MAYAHUDI HAWAISADIKI QUR_ANI TAKATIFU WALA HAWAMSADIKI MTUME (S.A.W.W

-:Mwenyeezi Mungu Mtukufu anasema

وَلَمَّا جَاءهُمْ كِتَابٌ مِّنْ عِندِ اللّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ وَكَانُواْ مِن قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلـَي الَّذِينَ كَفَرُواْ فَلَمَّا جَاءهُم مَّا عَرَفُواْ كَفَرُواْ بِهِ فَلَعْنَةُ اللَّه عَلـَي الْكَافِرِينَ[1]

Na kilipo wajia Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu kinacho thibitisha waliyo nayo - na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri - yalipo wajia yale waliyo kuwa wakiyajua !waliyakanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu juu ya wakanushao

Maelezo kuhusiana na Aya

Kabla ya kuja Mtume Muhammad (s.a.w.w.), Mayahudi walikuwa wakiwapa khabari Waarabu .[kuwa karibuni atadhihiria Mtume[2

Ama kusema kuwa hao Mayahudi walikuwa wakiomba kwa jaha ya Mtume, na wakishinda maadui zao kuwa ndio muradi wa Aya hii – maneno haya hawaakuyasema wale wafasiri wa mwanzo kabisa (salaf) wenye kutegemewa, kama Imam Ibn Jarir[3] Wala hawakuitaja vile vile .wale wafasiri wanaotegemea hadithi sahihi za Mtume

Imekuja katika qur-ani na hadithi sahihi kuombwa Mwenyeezi Mungu kwa majina yake, basi tufupizike na alivyotuambia Mwenyeezi mungu na Mtume wake. Wallahi hatutakuwa watovu .kwa kufupizika juu ya haya

-:Mwenyeezi anasema kuwaambia Mayahudi

لْ مَن كَانَ عَدُوّاً لِّجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلـَي قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللّهِ مُصَدِّقاً لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَهُدًى وَبُشْرَي لِلْمُؤْمِنِينَ[4]

Sema: “ Anayemfanyia ushinde jibril (kwa kuwa ndiye aliyemletea Utume Nabii Muhammad (s.a.w.w) asiwapelekee Mayahudi, (ni bure hana kosa jibril), hakika yeye ameiteremsha qur-ani

moyoni mwako kwa idhini ya Mwenyeezi Mungu, (sio kufanya kwa kupendelea kwake); (Qur-ani), inayosadikisha yale yaliyokuwa kabla yake, na ni uwongozi wa habari njema kwa .wanaoamini

-:Mayahudi katika hila zao za kumkataa Mtume Muhammad walimuuliza

-:Malaika gani anayekuletea wahyi? Mtume akasema“

Jibriyl”. Wakasema: “Lo! Huyu adui yetu, hatumtaki. Lau kama angelikuwa Malaika mwengine“ -:ndiye anayekuletea wahyi tungelikufuata.” Basi Mwenyeezi mungu anawajibu hivi

Suratul-Baqarah Aya ya 89 [1]

Tazama marejezo 18: 15-19, na yohana 1:25 [2]

.Tazama juzuu 2 iliyoshereheshwa na Shakir, ukurasa wa 332-335 hutaiona tafsiri hiyo [3]

Suratul baqara aya ya 97[4]

MWISHO